



Swahili Colloquium
Bayreuth



UNIVERSITÄT
BAYREUTH

KONGAMANO LA ISHIRINI NA NANE LA KISWAHILI

Tarehe 31 Mwezi wa Tano hadi tarehe 2 Mwezi wa Sita 2015

12 Novemba 2014

Wapendwa washiriki,

Tuna furaha kukukaribisheni katika Kongamano la ishirini na nane la Kiswahili hapa Bayreuth – *ama kwa wengi wetu tuseme karibuni nyumbani tena!*

Kongamano la Kiswahili

Kongamano hili la kila mwaka la Kiswahili limeshaota mizizi hapa katika Chuo Kikuu cha Bayreuth. Mwaka baada ya mwaka kongamano linawakaribisha wataalamu wa masomo mbalimbali wanaojishughulisha na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vinavyohusu Kiswahili na tamaduni zake. Upana wa mada zinazohusu Kiswahili na zinazozungumziwa kwenye Kongamano ni pana sana; nazo mada hizi ni kuanzia isimu, masomo ya fasihi mpaka anthropolojia, historia na jiografia, kwa kutaja chache tu, jambo ambalo linalipa kongamano hili msingi wa nguvu. Katika fursa hii wataalamu wanaojishughulisha na masomo anuwai kutoka pembe mbalimbali za dunia hupata kubadilishana mawazo. Wasanii, wahakiki na mashabiki wa fani mbalimbali za Kiswahili pia hujiunga nasi. Bali na furaha tuliyo nayo kuwakaribisha wale ambao wamezoea kuja hapa Bayreuth miaka iliyopita, tutafurahi kuwapokea na kuwakaribisha wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya, na wala yeyote asisite kupanga kuja.

Mada-kuu ya Kongamano la 2015

Kongamano la ishirini na nane litakuwa na mada-kuu ambayo twaiita: ***Linganisha! Mitazamo linganishi juu ya matumizi ya lugha, fasihi na tamaduni za Kiswahili.*** Kwa kuanza, fikira iletayo mtazamo huu inasababishwa na wazo lilengalo kuzingatia lugha, fasihi na utamaduni kama tukio la kijamii, na wala si miundo au vipengele vya kipekee: nao *mtazamo linganishi* huu unatuzalia njia mbili za kuiangalilia mada hii: Kwanza, kuzingatia kuwa Kiswahili kipo katika muktadha wa lugha na tamaduni mbalimbali Afrika ya Mashariki. Pili, kuangalia tofauti za lahaja, fasihi na tamaduni za Kiswahili katika mtazamo wa *kiutandawazi*, yaani kwa kulinganisha haya na utendaji wa isimu, fasihi na wa tamaduni nyingine kokote ulimwenguni ili kuweza kutenga kinachofanana na kilicho tofauti *kitaipolojia*.

Kuhusu namna ya kwanza ya kulinganisha Kiswahili katika muktadha wa Afrika Mashariki, tungependa kupendekeza mtazamo ambao kimsingi unasisitiza mahusiano ya Kiswahili na lugha, fasihi na tamaduni za lugha zingine za Afrika Mashariki, ili kwa kadiri yake, kuweza kushughulikia dhana ya upana wa muktadha na mseto wa lugha na tamaduni katika jamii za leo Afrika Mashariki. Badala ya kuchukua lugha ya Kiswahili kama mfumo imara wa isimu, tungependa kuangalia matumizi ya Kiswahili kwenye maisha ya watu Afrika Mashariki wanaozungumza zaidi ya lugha moja na wanaoishi katika tamaduni nyingi kwa kawaida. Masuala yanayoweza kuzuka ni: Je, miundo ya isimu, utamaduni na fasihi, kama

vile aina za usemi, zina uwiano au zinabishana kwa kiasi gani katika mazungumzo au mawasiliano? Je, fafanuzi za tanzu za fasihi na tamaduni zinaathiriana vipi na zinaathiri vipi kazi za waandishi wa fasihi na mashairi leo? Je, kwa kiasi gani shehena ya msamiati na uzoefu wa kutumia lugha zingine za kiasili na lugha za kikoloni (*repertoires*) zinaathiri Kiswahili na kwa jinsi gani Kiswahili kinabadilisha muundo wa lugha hizo pamoja na miundo ya lugha hizo *kisemantiki* na *kipragmatiki*? Kuna mabadilishano na mawasiliano yapi baina ya lugha, matini, waandishi, wahakiki na wataalamu; na je kuna mabadilishano yanayovuka mipaka ya nchi yanayohusisha lugha, fasihi na tamaduni mbalimbali?

Mada-kuu ya pili inalenga **ulinganishaji wa Kiswahili na isimu, fasihi na tamaduni za nje ya Afrika Mashariki**. Ingawa duniani ulinganishaji wa isimu na tamaduni kifasihi na jamii katika nyakati za baada ya uhuru zimekuwa zikiongezeka sana (na hata kuhusisha maeneo ya kusini), lugha na fasihi za lugha za Kiafrika hazijahusishwa sana. Ama kwa kweli, kuwahi kufanywa kwa ulinganishaji wa mambo haya kati ya lugha za kikoloni hasa na wataalamu wa Kiingereza au Kifaransa ni nadra, lakini utashangaa kugundua kuwa kulinganisha mambo yayo hayo, yaani kati ya Kiswahili na tamaduni nyingine za bara Afrika hayapatikani kabisa. Hivi basi yaelekea kuwa, *Mitazamo linganishi* ambayo ingeweza kuunganisha Kiswahili na dhana zingine za isimu na fasihi za Afrika na kwingineko haijazinduliwa bado. Masuala yazukayo hapa ni kama: Sifa za tanzu za usemi wa Kiswahili zinatofautishika vipi zikilinganishwa na lugha zingine kama vile Kizulu au Kiyoruba? Tanzu za fasihi, kama vile riwaya, zilichipuka vipi katika mazingira tofauti barani Afrika? Dhana ya heshima au tabia za fadhila inaathiri vipi mawasiliano ya Kiswahili tofauti na ifanyavyo katika lugha nyingine? Hadhi na mamlaka zimejengeka vipi katika jamii – kwa mfano, kijinsia au kimadaraka na kiumri – na zinaathiri vipi mawasiliano kwenye mazingira mbalimbali? Masuala ya ufahamu kuhusu ubunifu yanadai ulinganishaji kama: Dhana ya hisia inajengwa kwa njia gani katika Kiswahili kama ikilinganishwa na lugha zingine? Waandishi kutoka mazingira tofauti wanatumia mbinu zipi za kukumbana na matukio muhimu ya kihistoria kama vile kupata uhuru, na wanayaeleza vipi katika utunzi wao? Kwa kulinganisha Kiswahili na lugha zingine, kuna tofauti gani kati ya jinsi *mashirika ya kijamii* na *ya kisiasa* yanavyoathiri mawasiliano? Jukumu la uchapishaji na uhakiki wa fasihi ni lipi na usomaji wa fasihi unatofautiana vipi? Manufaa ya kutafsiri ni yapi? Waandishi wanaainishaje matini ili kuafikiana na aina za vyombo vya habari na *teknolojia*?

Hata ingawa mitazamo ya ulinganishaji yatakuwa chanzo au *kipengele-kati* cha mijadala yetu katika kongamano lijalo, si kwamba hatutaangalia na kuzingatia mapendekezo yenye mada nyinginezo; ilimradi Kongamano la Kiswahili lina nia ya kukuza mijadala inayohusisha nyanja tofauti, na hivi basi, kongamano hili ni fursa iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayokihusu Kiswahili.

Kujiandikisha

Tunawaulizeni mtutumie makala zenu katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza. Kila uwasilishaji wa mada utapewa muda wa dakika 20 na dakika kumi za majadiliano, yaani jumla ya dakika 30 tu. Tafadhali jiandikisheni mapema iwezekanavyo (mpaka kufikia tar. 22 Novemba 2015) kwa kututumia baruapepe (swahili@uni-bayreuth.de) ambamo mtatutumia **kichwa cha makala** yenu. Tunawaomba hata wale ambao hawatatoa makala wajandikishe. Tuna haraka hivi kwa sababu tunahitaji kuandika ratiba na makadirio ya kongamano ili tuweze kuomba ufadhili wa kifedha. Tafadhali kisha mtutumie muhtasari wa makala yenu mpaka kufikia tar. 10 Februari 2015. Iwapo utawasilisha makala yako kwa Kiswahili, tunauliza utuandikie ufupisho wake pia kwa Kiingereza.

Pahala/Wakati

Kongamano hili litafanyika *Iwalewa-House mpya*, jumba la masomo ya Kiafrika la Chuo Kikuu cha Bayreuth. Hivi majuzi jumba hili limehamia Wölfelstraße 2; hatua chache tu kutoka *Iwalewa* ya awali.

Kongamano la Kiswahili la 2015 litaanza Jumapili tar. 31 Mei na litamalizika Jumanne tar.2 Juni. Wakati huu umechaguliwa kwa sababu mbili; Kwanza, *Iwalewa-House* itafunguliwa upya rasmi na

kutakuwa na maonyesho kuhusu nchi ya Kenya tar. 30 Mei. Pili; baada ya Kongamano la Kiswahili, mkutano wa Changamano la Fasihi za Kiafrika (*African Literatures Association*) utafanyika mjini Bayreuth kuanzia tar. 3 hadi tar. 6 Juni 2015. Kichwa cha mkutano huo, ambao pia mnakaribishwa kuuhudhuria, ni “African Futures and Beyond. Visions in Transition.” Mnaweza kutuma makala mpaka tar. 30 Novemba 2014. Kwa maelezo zaidi tazama: <http://www.ala2015.com>

Mwanzoni mwa 2015 tutawatumieni barua ya pili ya mwaliko itakayotoa habari kuhusu ratiba na maelezo mengine, kama vile suala la malazi. Yeyote aliye na swali au jambo, asisite kuwasiliana nasi; mambo yanayohusu kongamano tafadhali tumieni anwani yake: swahili@uni-bayreuth.de

Tukiwa na matumaini ya kuonana katika Kongamano la ishirini na nane la Kiswahili hapa Bayreuth – twasema: *Karibuni sana!*

Prof. Dr. Clarissa Vierke
Literatures in Afrikan Languages
University of Bayreuth,
95440 Bayreuth

Simu: +49-921-553550
Faksi: +49-921-553641
Barua pepe: swahili@uni-bayreuth.de